22102841

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Friday 21 May 2010 (afternoon)
Vendredi 21 mai 2010 (après-midi)
Viernes 21 de mayo de 2010 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.





© International Baccalaureate Organization 2010

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

## UNGEPENDA KUONA NINI? KARIBU SANA!

Yafuatayo ni matangazo ya matukio (*events*) mbalimbali ya sanaa na utamaduni jijini Dar es Salaam.

**Tingatinga: Twende Pamoja**
Picha mbalimbali za Tingatinga
**Maonyesho Tarehe**: 20-30 Juni
**Mahali**: Galari ya Mawazo
Hakuna kiingilio



**SUKARI YA KAHAWIA**
**Maonyesho ya vinyago na picha za wasanii wa Tanzania na wa Spain.**
*Hotuba ya kufungua: Balozi wa Spain nchini Tanzania*
**Mahali**: Galari ya Mawazo
**Hakuna kiingilio**
**Tarehe**: 30 Juni hadi 7 Julai

**WASANII WATATU**
*Maonyesho ya wasanii watatu wa Tanzania: David Mzugano, Joseph Chigege na Saidi Mbaraki*
**Mahali**: Kituo cha Sanaa cha Wasanii.
**Kiingilio**: Bure
**TAREHE**: 7 hadi 17 Julai

**MWISHO/*LIMITATIONS***
Dansi ya kisasa itachezwa na "Mionzi Dance Theatre" kutoka Tanzania, na "CE Dance" kutoka Sweden. Camilla Ekelof ataonyesha ufundi wa kucheza kwa kutumia sauti za viatu alivyovaa. Kwa vile haya bado ni mazoezi kila mtu anakaribishwa. **Kiingilio** ni bure.
**Mahali**: Ukumbi wa Nkrumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; **Tarehe:** 18 na 19 Julai

**FILAMU 4 ZA KITANZANIA**
*Oprah, Machozi katika Familia, Regina na Hakuna Kurudi Nyuma!* Njoo uwaone waigizaji maarufu wa filamu Tanzania: Akina Kanumba, Ray, Irene Uwoya, Wema Sepetu na wengi wengine
Saa 9.00–11.30 jioni, Saa 12.00–1.30 usiku,
Saa 2.00–3.30 usiku, Saa 4.00–5.30 usiku.
**Tarehe**: 18–30 Julai. **Kiingilio**: Shilingi 3000
**Mahali**: Ukumbi wa Senema wa Century, Mlimani City.



Kutoka *Dar Life* (Februari 2009)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

## UNGEPENDA KUSAFIRI KWENDA WAPI?



Tunafurahi kuwatangazia ratiba yetu ya safari za ndege kutoka Nairobi kwenda miji mbalimbali duniani wakati wa kiangazi. Huu ni wakati ambapo nauli ni za bei nafuu kuliko wakati mwingine wowote, na ukiwahi kufanya buking utapata tiketi kwa urahisi sana. Pia, kwa wale ambao wanasafiri mara kwa mara, watapewa punguzo (*reduction*) la nauli pamoja na kulipiwa gharama za hoteli katika miji ambayo imewekewa alama ya nyota (*). Punguzo hili si kwa mwaka mzima, ni wakati wa kiangazi tu. Kuna punguzo maalumu pia kwa watoto, wanafunzi, na wale ambao wanaenda fungate (*honeymoon*). Karibu ufurahie raha ya kusafiri katika ndege zetu kubwa na za kisasa. Njoo upate ukarimu wa Kiafrika. Usafiripo nasi utapumzika, hutachoka. Kama upo Nairobi piga simu namba +254 722 009 007 tutakupatia ratiba yetu vizuri. Ifuatayo ni ratiba ya safari za ndege za shirika letu. Safari zote zinaanzia Nairobi.

| Kutoka Nairobi Kwenda... | Nauli Wakati Wa Bei Nafuu | Mara Ngapi Kwa Siku / Wiki | Tarehe Za Kufanya Buking | Tarehe Za Kusafiri |
|---|---|---|---|---|
| | 11 Jan – 13 Juni<br>01 Sept – 03 Des. | | | |
| Addis Ababa | $760 | Mara 4 kwa wiki | Machi 1 - Mei 30 | Juni 10 – Sept 31 |
| Atlanta | $1297 | Siku 4 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Boston | $1191 | Siku 5 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Cairo | $840 | Siku 5 kwa wiki | Machi 20 – Mei 10 | Mei 15 – Sept 30 |
| Chicago | $1262 | Siku 4 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Dakar | $1050 | Siku 1 kwa wiki | Machi 20 – Mei 10 | Mwezi wa Agosti tu |
| Dar es Salaam | $490 | Mara 3 kila siku | Machi 20 – Mei 10 | Mei 15 – Jan 15 |
| Detroit | $1319 | Siku 6 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| London | $900 | Siku 6 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Mombasa | $260 | Mara 4 kila siku | Januari 1 – Apr 30 | Mei 1 – Des 03 |
| New York | $1191 | Siku 6 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Kisumu | $200 | Siku 2 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Washington (IAD) | $1268 | Siku 7 kwa wiki | Mei 1 – Juni 30 | Julai 31 – Sept 30 |
| Zanzibar | $510 | Mara 2 kila siku | Machi 20 – Mei 10 | Mei 15 – Des 03 |

**KARIBU UPANDE NDEGE NA SISI!**

Imechotwa na kurekebishwa kidogo kutoka *http://www.takimsholidays.com/flights/index.asp*



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

## KISWAHILI AU KIINGEREZA KATIKA ELIMU?

***Hayo hapo chini ni mawazo ya wanafunzi kuhusu lugha ya kufundishia katika elimu ya sekondari na chuo kikuu. Je, iwe ni Kiswahili au Kiingereza?***

***Abdul Taibar***
Ninasoma shule ya sekondari. Ninafikiri lugha zote mbili, Kiingereza na Kiswahili ni nzuri kufundishia kwa sababu zote ni muhimu sana katika maisha yetu.

***Josia Makaranga Elias***
Ninasoma shule ya sekondari. Kiingereza kinafaa kuendelea kuwa lugha ya kufundishia sekondari na vyuoni. Wazazi wangu wanasema kuwa Kiingereza kitanisaidia katika maisha; kwa mfano kitanisaidia kupata marafiki wengi kutoka nchi nyingine duniani ambao hawawezi kuzungumza Kiswahili. Nitajua utamaduni wao na wao pia watajua utamaduni wangu.

***Furaha Muselem***
Waalimu watumie lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza. Hii itawasaidia wanafunzi wote kwa sababu wale ambao walisoma shule ya msingi kwa Kiingereza sasa wataanza kuelewa Kiswahili, na wale ambao walisoma shule ya msingi kwa Kiswahili sasa wataanza kuelewa Kiingereza vizuri.

***Tumpale Mwakalinga***
Mimi nafikiri ni vizuri masomo yafundishwe kwa Kiingerza tu, na wanafunzi wote lazima wajifunze Kiingereza vizuri sana. Mimi sasa hivi ninasoma masomo yote katika shule ya msingi kwa Kiingereza, na ninajua nitapata maisha mazuri sana baadaye.

***Elizabeth Kiondo***
Ninataka masomo yote katika sekondari na vyuoni yafundishwe kwa Kiswahili tu kwa sababu ni lugha ya tangu utotoni, yaani ni lugha yetu ambayo tunaijua tangu tukiwa watoto. Pia wazazi wetu wanaijua lugha hii kwa hiyo watatusaidia katika kazi za nyumbani (*homework*). Wanafunzi wengi wanapata shida kuelewa masomo kwa sababu yanafundishwa kwa Kiingereza – lugha ya kigeni ambayo hawaielewi kabisa.

Kutoka *The Guardian, Jumapili* (Novemba 2008)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

## MAISHA YA MWANAMUZIKI



Sisi ni wanamuziki kutoka Kenya. Maisha ya mwanamuziki yana raha na tabu zake. Hayatofautiani sana na ya mwanafunzi. Kama wewe ni mwanamuziki lazima ufanye bidii sana kutunga muziki, kufanya mazoezi mengi, na pia kusikiliza muziki wa waimbaji wengine.

Raha ya kuwa mwanamuziki ni pale unapokuwa mbele ya watu, hasa vijana, halafu wanashangilia wakati unaimba. Mashabiki (*fans*) wanapofurahia nyimbo na muziki wako basi unapata raha sana.

Lakini pia, kuwa mwanamuziki kunahitaji kuwa na nidhamu. Ni vizuri kupanga ratiba vizuri ujue unalala saa ngapi, unaamka saa ngapi, unakula saa ngapi, unafanya mazoezi saa ngapi, unaenda sehemu za burudani saa ngapi, unafanya maonyesho saa ngapi na unalala tena saa ngapi.

Pamoja na yote, kama wewe ni mwanamuziki, lazima ujue pia kuwa una familia – baba na mama, na labda mke au mume, na watoto. Wote hawa ni sehemu ya maisha yako, na ni lazima uwape nafasi na muda katika ratiba yako.

Kuwa mwanamuziki si uhuni. Muziki ni kazi sawa na kazi nyingine kama vile udaktari, ualimu, uhandisi au hata urubani wa ndege. Muziki ni shughuli ambayo inakupatia pesa na kukufanya uishi vizuri. Pia muziki unaweza kukufanya utembelee sehemu mbalimbali duniani na kujuana na watu wengi sana.

Kutoka *Msafiri – The Traveller, Jumapili* (Januari 2008)



https://xtremepape.rs/